# Kulijenga Upya Taifa Letu kwa Utawala Shirikishi na Unaowajibibika




**... Haya! Na Tuanze Kazi ya Kulijenga Upya Taifa Letu (Nehemia 2:17-18)**

*Kampeni ya Kwaresima 2021*

S.L.P. 13475-00800, Nairobi
Waumini House, Westlands
Simu: (254-20) 4443133/4/5, 4443917
Barua pepe: national@catholicchurch.or.ke
Tovuti: www.cjpc.kccb.or.ke
www.kccb.or.ke

YOU SHALL BE MY WITNESSES K.C.C.B

CJPC

© KCCB -Tume ya Kikatoliki ya Haki na Amani
Mwaka wa kuchapishwa: 2021

Afisi Kuu ya Baraza la Maaskofu Wakatoliki wa Kenya
Tume ya Kikatoliki ya Haki na Amani
Waumini House, Westlands
S.L.P. 13475-00800, Nairobi
*Simu:* (+254) 20 444112/4443906 au 722 457114
*Barua pepe:* national@catholicchurch.or.ke
*Tovuti:* www.cjpc.cjpc.or.ke
www.kccb.or.ke

Ubunifu na utayarishaji
KCCB-Tume ya Kikatoliki ya Haki na Amani

*Wahariri*: Beatrice Odera, Grainne Kidakwa na Wainainah Kiganya
*Mchoraji*: Robert Kambo
*Msanifu na mpambaji wa kurasa:* Monicah Nyambura
*Waratibu wa michango:* Margaret Mkavita and Eunice Nderitu

Kimepigwa chapa na Don Bosco Printing Press
S.L.P. 158 Makuyu 01020, Kenya

# Yaliyomo


## Sala

Tukate Mnyororo ya Ufisadi....4

## Dibaji

Kulijenga upya taifa letu kwa utawala shirikishi na unaowajibika ....5

## Utangulizi

Kwaresima katika Kanisa Katoliki ....10

## Wiki ya Kwanza

Familia....12

## Wiki ya Pili

Vijana, tegemeo letu la siku zijazo....16

## Wiki ya Tatu

Ufisadi na ufufuaji wa uchumi ....21

## Wiki ya Nne

Usalama ....27

## Wiki ya Tano

Usimamizi wa mazingira na udhibiti wa majanga ....32

## Kiambatisho

Michango ya Kampeni ya Kwaresima ya 2020 ....37

# NA TUUVUNJE MNYORORO WA UFISADI

Baba yetu uliye mbinguni, umekuwa ukijali viumbe vyako vyote ili tuishi kulingana na mapenzi yako. Umeibariki nchi yetu kwa watu wenye vipawa vingi na kutupatia mali asili za kutumiwa kwa sifa na utukufu wako na kwa manufaa ya kila Mkenya.

Tunahuzunishwa sana na utumiaji mbaya wa hizi zawadi na baraka zako kwetu kupitia kwa tendo la ufisadi ambalo limesababishia watu wengi njaa, magonjwa, kuwanyima makao na kuwafurusha makwao, kuwaacha wengi bila elimu na kinga yoyote maishani. Baba, ni wewe pekee uwezaye kutuponya kutokana na ugonjwa huu ambao hatima yake ni mauti.

Tunakusihi uguse maisha yetu na ya viongozi wetu ili tutambue uovu wa ufisadi na kujitahidi kikamilifu kuliangamiza jinamizi hilo. Kwa raia yeyote ambaye amejipatia chochote kifisadi, Bwana, mpe nguvu na ujasiri wa kukirudisha na kukurejelea.

Tunakuomba utupe raia wanaomcha Mungu na viongozi wanaotujali na ambao watatuongoza katika njia ya amani, haki, ufanisi, maendeleo, na la muhimu zaidi, upendo.

Tunaomba hayo kupitia kwa Kristo Bwana wetu.

**Ee Bwana tunakuomba utusikie.**

# Dibaji

## Kulijenga Upya Taifa Letu kwa Utawala Shirikishi na Unaowajibika ... Haya! Na Tuanze Kazi ya Kulijenga Upya Taifa Letu (Nehemia 2:17-18)

Kulijenga upya taifa letu ni kazi na wajibu wa kila Mkenya. Tunazo pande mbili za kauli hii. Kwa upande mmoja, hatuna budi kuanza kufuata taratibu mpya za maisha kutokana na nafasi mpya zinazoletwa na maendeleo katika nyanja za maarifa na teknolojia. Kwa upande mwingine, maendeleo katika utambuzi na teknolojia yanaleta changamoto mpya ambazo hatuna budi kuzikabili. La muhimu zaidi katika Kampeni ya Kwaresima ya mwaka huu ni maudhui ya utawala shirikishi na unaowajibika. Tunapendekeza kwamba tuangazie maudhui haya tukiegemea misingi ya kujenga na kukuza maadili. Tunatambua kwamba pasina misingi thabiti ya kujenga maadili, ni vigumu kupata utawala shirikishi na unaowajibika. Kujenga maadili ndio msingi wa safari ya utakatifu ambao Wakristo wote na watu wengine wenye mapenzi mema hualikwa kuufikia kupitia kwa sakramenti, kuwapenda majirani na kusimamia kikamilifu zawadi zote ambazo Mungu ametupatia.

### Kujenga maadili: Mwito wa utakatifu

Yaonekana tukiwa nchi tumepoteza dira ya maadili. Uadilifu ni itikadi ya maadili na kanuni ya utawala ambayo ikiheshimiwa hutusaidia kutambua haja ya kujitolea kuwahudumia wengine kwa uaminifu bila kujali tabaka ya kijamii ya mtu. Kristo ameeleza kwa kifupi mafunzo kuhusu uadilifu anapotwambia kwamba: “Kila kitu mlichomtendea mmojawapo wa hawa ndugu zangu wadogo, mlinitendea mimi” (Mathayo 25:40). Matendo na kazi zetu zinafaa kubaini uaminifu, uwajibikaji na uwazi, kwani kwa njia hii tutakuwa tunahudumiana kama ndugu na dada wa Mungu mmoja.

Katika Kampeni ya Kwaresima ya mwaka huu, tunaangazia suala la kujenga maadili. Kristo anatualika tuwe watakatifu katika maisha yetu ya kila siku. Hii ni safari ambayo Roho Mtakatifu anaandamana nasi. Mtakatifu Paulo, kupitia kwa maisha na nyaraka zake, anatukumbusha

kuwa safari hii ya utakatifu inahitaji kujitolea kikamilifu kwa lengo kuu: kuungana na Baba mbinguni. Kwa njia maalumu, tunaangazia kujenga maadili katika kampeni hii ya Kwaresima kwa sababu ya mafunzo tunayoyapata maishani, kama vile vitisho kwa familia, kesi zinazotia hofu za mimba za matineja, kuwatumia vijana kuzusha fujo za kisiasa, ufisadi ulioenea kote, kuzorota kwa hali ya usalama katika baadhi ya maeneo ya nchi na mazoea ya kuvunja upendo na umoja nchini, mambo ambayo ni muhimu kwa familia ya Mungu.

Kwa sababu hii, mada za kila wiki zinaambatana na waraka wa kichungaji uliotolewa na maaskofu mnamo Februari, 2020, katika Subukia Shrine, Jimbo la Nakuru. Tunahimiza kwamba Kampeni ya Kwaresima ya mwaka huu itusaidie kutafakari, kusali na kuzingatia kufanya yaliyo sahihi mbele ya Mungu. Tunaitwa kwa utakatifu kwa njia zetu ndogo kwani hivyo ndivyo Mungu huzungumza nasi; jinsi tulivyo.

## Wiki ya Kwanza: Utakatifu kwenye familia

Familia ndiyo nguzo kuu ya jamii. Ukweli ni kwamba familia ndiyo Kanisa ya nyumbani. Msingi wake ni Amri ya Tano. Watoto wasipojifunza kuheshimu wazazi wao, huwa wanakosa msingi wa wema wa heshima na hivyo basi huwa hawaheshimu mamlaka yoyote. Familia inapogeuzwa kuwa mandhari ya matendo maovu na ya kumchukiza Mungu, hatimaye jamii yote itaathirika. Mtakatifu Teresa wa Calcutta, anayejulikana na wengi kama Mama Teresa, alionya kuwa: “Tukikubali kwamba mama anaweza kuua mtoto wake, tutawezaje kuwaambia watu wengine wasiuane?” Chanzo cha matatizo yetu ya kijamii ni kuvunjika kwa familia.

## Wiki ya Pili: Utakatifu katika kujenga maadili ya vijana

Limekuwa ni jambo la kusikitisha kukuta vijana wengi waliohitimu mafunzo katika ngazi tofauti wakikatishiwa tamaa na kuvunjwa moyo na uhaba wa nafasi za kazi. Huenda hali hii ikawa kama bomu linalosubiri wasaa wa kulipuka. Ni wajibu wetu kuwapatia vijana matumaini. Serikali za kaunti na kitaifa zina jukumu la kuangazia kwa njia maalumu miradi na shughuli zinazowapatia vijana matumaini na kuwawezesha kutimiza ndoto zao. Mazoea ya kutoa nafasi za kazi kwa wazee na wakati mwingine viongozi waliostaafu huwaudhi zaidi vijana. Mnamo siku za karibuni, tumeshuhudia matendo ya vijana waliokata tamaa maishani, suala ambalo hatuna budi kuliangazia. Tukiwa waumini wa Kanisa na wazalendo,

lazima tuchukue hatua thabiti kushauri, kutoa nasaha, kuandamana na kuwasaidia vijana wenye vipawa na ujuzi ili kupata ajira na njia za kujipatia riziki. Hatua hizo ni pamoja na kuwaelimisha kuhusu njia zinazozidi kufunguka za kujipatia mapato kufuatia kurahisishwa kwa utoaji mikopo.

Wiki hii, tunaangazia jinsi vijana wanavyotamani kujengwa kimaadili na kiroho. Vijana walioundika kikamilifu ni nguzo muhimu ya jamii yoyote. Kujengwa kiroho huwasaidia vijana kuchukua maamuzi yafaayo na yanayobaini imani yetu tukiwa Wakatoliki. Isitoshe, wakiundika kikamilifu kimaadili na kiroho, vijana hutambua umuhimu wa bidii, uaminifu, uadilifu, kuzalisha mali na huwasaidia wazazi wao, walezi na ndugu zao. Hawa ndio vijana ambao huwa hawasubiri kuhudumiwa, ila lengo lao huwa ni kuwasaidia wengine, sawa na alivyofanya Kristo. Ina maana vijana hujifunza kuwa Wakristo wanaowajibika na kuonyesha dhahiri mapenzi ya Mungu kwao na kwa wengine walio karibu nao.

## Wiki ya Tatu: Utakatifu katika kuukata mnyororo wa ufisadi

Ufisadi katika nchi yetu umefikia kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa. Umesababisha vifo vingi, mateso na hata kukatisha wengi tamaa. Ufisadi umejibainisha pia kwa ukosefu wa dawa na vifaa muhimu vya matibabu hospitalini, muundo msingi duni, vifo kutokana na ajali barabarani za motokaa na pikipiki, uhaba wa maji safi ya kunywa, maafa kutokana na njaa na uhaba wa nafasi za kazi kwa vijana ambao hawana uwezo au hawataki kutoa hongo. Yasikitisha kukuta rasilmali zilizotengewa manufaa ya wote zinaishia kunufaisha maslahi ya kibinafsi.

Ili kupigana na ufisadi, tunao wajibu wa kinabii wa kushutumu aina zote za ufisadi, jukumu ambalo ni wito wa utakatifu wa kutetea ukweli. Changamoto kubwa ya kijamii inayotukabili Kenya ni mazoea ya kuchukia ukweli katika vita ya ufisadi. Ukweli ni tunu na thamani yake ni kubwa. Ukweli ndio msingi wa uhusiano wetu na Mungu na majirani; ni nguzo ya sheria zote za maana. Bwana wetu Yesu alitufunza kwamba “ukweli utatukomboa”. Ukweli huu ni hali ya Mungu na mpango wake mtakatifu.

Ufisadi sio manufaa ya kifedha pekee, la hasha! Unahusu pia ‘kukata kona’ katika taratibu zinazokubalika za kufanya mambo, kutojali utu na kuchukua maamuzi kwa manufaa ya kibinafsi. Ufisadi hutufunga macho tusiuone ukweli wa aina yoyote. Viwango vya juu vya umaskini, kutoaminiana, upendeleo wa kiukoo, fujo, mauaji, uuzaji wa watu utumwani, mizozo ya kikabila, upendeleo wa marafiki wa karibu na

jamaa, na utumiaji mbaya wa pesa za umma ni ishara za uozo ulioenea kwenye taratibu zetu za jamii na vile tulivyopoteza dhamiri tukiwa jamii. Changamoto yetu kubwa ni vile ufisadi umeenea katika taratibu zote za maisha na miongoni mwa watu binafsi.

Ndiposa mizozo katika jamii, ufisadi, mivutano ya kisiasa, tabia za kichokozi miongoni mwa vijana, kutojali kuadhibiwa katika shughuli za binafsi na za umma inatokana na mazoea ya kutothamini ukweli maishani. Tunalo tatizo la maisha ya kinafiki kwa sababu hatutaki kuwa wakweli wa hali zetu halisi. Hatuwezi kufanikiwa kupigana na ufisadi iwapo tutaukinai ukweli.

Kwa bahati mbaya, ufisadi hujitetea. Sawa na ilivyokuwa nyakati za Judasi, wafuasi wengi wa Yesu walimtoroka alipokabiliwa na maadui wa ukweli na haki. Wakenya tumefanya hivyo pia tunapohitajika kutetea ukweli katika vita vya ufisadi. Hata hivyo, wasaa ndio huu wa kuonyesha ujasiri mpya. Wasaa ndio huu wa kumwangamiza nduli huyo, sio kwa ncha ya upanga lakini kwa ujuzi na tukimwamini Mungu.

Ndiposa sote tunaalikwa kuponya na kukomboa dhamiri zetu. Ufisadi ni njia ya mauti kwa binadamu, kama alivyotukumbusha Baba Mtakatifu Francis kwenye hotuba yake kwa vijana katika uwanja wa kimataifa wa Kasarani, Nairobi, mnamo Novemba, 2015. Sawa na Zakayo mkusanyaji ushuru (Luka 19:1–10), ni lazima tukubali kuwa tumepotea njia kwa kunyakua mali zisizo zetu na kumwomba Mungu msamaha.

Wiki hii, tunaangazia hatua ambazo kila mmoja wetu anaweza kuchukua kupigana na ufisadi. Jukumu la Kanisa ni kuwa dhamiri ya jamii. Hili linatilia mkazo wajibu wa Kanisa katika kuzijenga dhamiri za watu wote ili watende yaliyo sahihi na kutambua umuhimu wa manufaa kwa wote. Sote tunapaswa kuongozwa na dhamiri thabiti katika shughuli zetu zote na kila tunapochukua maamuzi. Jamii adilifu inaweza kupatikana tukiwa na wanaume na wanawake waadilifu. Haki na usawa zinaweza kupatikana tukiimarisha imani yetu kwa Mungu na kuungana na Daudi katika vita hii ya kumwangamiza Goliatho. Mataifa mengi ulimwenginе yamefaulu kuangamiza ufisadi na sisi tunaweza pia.

## Wiki ya Nne: Jukumu la kuimarisha usalama kwa wote

Vitishio kwa usalama wa Kenya vimeendelea kuongezeka. Tumeshuhudia mashambulizi ya kigaidi na ongezeko la visa vya fujo nyumbani na kwenye familia. Baadhi ya sababu kuu za kuzorota kwa usalama ni mafunzo ya

itikadi kali na kutovumiliana, utumiaji mbaya wa teknolojia za kisasa, uhamaji na usafiri wa watu kote duniani na uhaba wa mali asili nchini na katika mataifa jirani. Hata hivyo, uwezo wetu kutosheleza mahitaji yetu ya usalama umeongezeka kwa viwango vya kuridhisha. Usalama ni haki ya raia wote. Tunaamini kwamba hatua thabiti zinaweza kutekelezwa kuimarisha usalama kwa manufaa ya taifa.

### Wiki ya Tano: Kuupata utakatifu katika yaliyo ya manufaa kwa wote

Manufaa kwa wote ni kanuni ya mafunzo ya jamii ya Kikatoliki na hutajwa kuwa jumla ya hali za jamii zinazowawezesha watu wakiwa makundi au binafsi, kutosheleza mahitaji yao. Huwaongoza watu kuhusu jinsi wanapaswa kuishi na wengine. Hutilia mkazo umuhimu wa binadamu kama nguzo kuu ya juhudi zozote za kibinadamu na hutukuza mahusiano ya binadamu. Baba Mtakatifu Francis kwenye waraka wake *Makao yetu sote* (*Laudato Si)*, amefafanua majukumu yetu tukiwa Wakristo na binadamu kutunza mama wetu ardhi. Amewahimiza watu wote kubeba jukumu la kuhifadhi na kuimarisha sifa ya ulimwengu wetu. Mabadiliko makuu ya hali ya hewa ni tishio kwa mamilioni ya familia zinazotegemea kilimo cha mazao ya chakula na ufugaji. Matendo ya wanadamu kama vile kukata miti, kuchafua mazingira, kuchimba na kutumia madini kiholela ni mambo yanayoyapunguzia makao yetu sote tunu za kudhibiti maisha. Makao yetu sote ni manufaa kwetu sote na kila mmoja ana wajibu wa kuyaimarisha.

Tunapoliangazia suala la kulijenga upya taifa letu kwa utawala shirikishi na unaowajibika, tufanye hivyo kwa moyo wa Kwaresima, msimu ambao ni wa kusali, kufunga na kuwasaidia maskini.

Nawatakieni nyote msimu wa Kwaresima uliojazwa Roho wa Mungu na wenye mafao.



**Askofu John Owaa Oballa wa Jimbo la Ngong'**
**Mwenyekiti, Tume ya Kikatoliki ya Haki na Amani**

# Utangulizi

## KWARESIMA KATIKA KANISA KATOLIKI

Kwaresima ni kipindi cha siku 40 cha kufunga na kujinyima, kusali na kutubu kabla ya Pasaka. Kulingana na utamaduni wa Kikristo, msimu huu katika mwaka wa kiliturjia huanza Jumatano ya Majivu na kumalizika Jumapili ya Matawi. Ni adhimisho la kila mwaka ambalo huwatayarisha waumini — kupitia sala, toba, kutoa zaka na kujinyima — kwa matukio yanayohusiana na mateso ya Yesu msalabani, na maadhimisho ya ufufuko wake. Wakatukumeni hubatizwa Jumapili ya Pasaka.

### Kwa nini siku 40?

Nambari 40 ni muhimu katika maisha ya Wakristo. Musa na wana wa Israeli, kwa mfano, walitanga jangwani kwa miaka 40 wakijiandaa kwenda katika nchi waliyoahidiwa na Mungu. Musa alikaa juu ya Mlima Sinai kwa siku 40 bila kula wala kunywa alipokuwa ameenda kupokea vibao vya mkataba ambao Mungu aliwawekea Waisraeli. Nyakati za Nuhu, gharika iliendelea kwa siku 40 mchana na usiku. Eliya alikaa siku 40 mchana na usiku juu ya Mlima Horebu bila chakula. Yesu naye aliendа jangwani na kufunga kula na kunywa kwa siku 40 mchana na usiku.

### Asili ya Kampeni ya Kwaresima Kenya

Kuzingatia wito wa kiroho wa msimu wa Kwaresima, Kanisa Katoliki katika Kenya liliazimia kuwapasha waumini habari kuhusu matatizo yanayokumba jamii na kushirikiana nao kutetea mabadiliko. Kupitia kwa Kampeni ya Kwaresima, Maaskofu wa Kanisa Katoliki huwaita Wakristo wote na watu wa mapenzi mema kuungana na kukabiliana na matatizo hayo, huku wakitetea mabadiliko. Kwa kuungana na maaskofu katika utetezi huo wa mageuzi, juhudi za kila mtu binafsi pamoja na sauti ndogo ya kila mmoja ikiunganishwa na ya wengine husikika mbali, nayo matendo ya kila mmoja huongezeka yakijumuishwa na ya wengine.

# Wiki ya Kwanza

FAMILIA



## FAMILIA

### Tazama: Simulizi

Tarajio na Subira walikutania chuoni wakiwa wanafunzi. Baada ya kuhitimu masomo yao, kila mmoja alipata kazi. Uhusiano wao wa kimapenzi ukanawiri, wakafunga ndoa na hatimaye wakapata watoto wanne; Zawadi, Faith, Prince na Charlo. Maisha yalikuwa mazuri na ya furaha kwa familia hiyo changa. Waliandamana kwenda kanisani, kujivinjari na hata kwenda madukani wikendi.

Kadiri siku zilivyosonga ndivyo gharama ya maisha ilizidi kupanda. Matumizi ya kila siku ya familia ya Tarajio na Subira yaliongezeka kiasi kwamba mishahara yao haikutosha kuwawezesha kujikimu. Mume na mkewe wakalazimika kutafuta jinsi ya kujipatia mapato ya ziada. Ajira mpya iliwalazimu kukaa nje kwa saa nyingi kila siku, ikiwa ni pamoja na wikendi. Familia ilivyozidi kunawiri kifedha ndivyo wazazi waliendelea kuwapuuza watoto wao. Familia haikuwa na nafasi tena ya kwenda kanisani pamoja. Ikawa ni nadra sana kwa wazazi kufuatilia elimu ya watoto wao wala kupiga msasa tabia na maadili yao.

Kadiri mapato yao yalivyoongezeka, ndivyo Tarajio na Subira walivyoamini kwamba kutokuwepo nyumbani kwa muda mrefu kulikuwa ni kwa manufaa ya familia. Katika kujaribu kuthibitisha jinsi walivyowajali na kuwapenda watoto wao, na wakati huo huo kuziba pengo la kutokuwepo nyumbani, wanandoa walinunua vifaa vya kisasa vya kieltroniki kama kompiuta za saizi tofauti, mashini za michezo, simu za mikononi na kuleta huduma za *Internet* nyumbani. Vifaa vyote hivyo viliwafungulia watoto mambo yaliyozorotesha maisha yao. Zawadi na Prince wakajitosa kwa kamari, ukahaba na dawa za kulevya. Zawadi alipachikwa mimba.

La kusikitisha ni kwamba Tarajio na Subira hawakuwa na habari kuhusu yaliyowafika watoto wao. Siku moja, babu na nyanya wa kuumeni wa watoto hao wakiwa njiani kumtembelea rafiki yao jijini, walifika ghafla nyumbani kwa Tarajio na Subira. Haikuwachukua muda wazee hao kutambua kasoro bomani mwa watoto wao. Zawadi, Prince na wazazi wao hawakuwepo. Wajukuu wengine walikuwa wakicheza na kompiuta na simu. Wazee wakaachwa kujitumbuiza kwa kutazama televisheni.

Zawadi alirudi nyumbani saa tano za usiku akiwa mlevi chakari. Babu na nyanya yake walishangaa kwamba mjukuu wao hakuonekana kubabaishwa na hali yake wala saa alizofika nyumbani. Muda mfupi baadaye, Prince alifika akiandamana na vijana wengine walevi na wakorofi.

Baada ya mashauriano ya muda na wajukuu wao, nyanya akagundua Zawadi alikuwa mja mzito ilhali Prince alishakuwa mlevi mzoefu.

Tarajio na Subira walirudi nyumbani baada ya usiku wa manane na kushangaa ni kwa nini taa hazikuwa zimezimwa. Mara moja wakahisi mambo hayakuwa shwari. Kufungua mlango wa nyumba, Tarajio alikuta wazazi wake waliojawa na huzuni wakishauriana na wajukuu wao. Tarajio na Subira hawakuyaamini waliyoyasikia na kushuhudia. Ikawa ni kulaumiana. Tarajio akamlaumu Subira kwa yote yaliyowakumba watoto wao, akidai kwamba jukumu kubwa la kulea watoto lilikuwa ni la mama, huku baba akiitafutia familia riziki. Mabishano makali kati ya Tarajio na mkewe yalizimwa na wazee wao. Tarajio akawageukia Zawadi na Prince kwa makofi na mateke akiwasuta kwa kuaibisha familia yake. Babu na nyanya walituliza mambo.

Wazazi wake Tarajio waliitisha kikao cha familia ya mwanao na wakawapa wote fursa ya kufungua roho. Kupitia kwa baba paroko, washauri wa masuala ya familia na ndoa walialikwa kuwashauri Tarajio, Subira na watoto wao. Baada ya vikao vingi vya ushauri na sala, Prince na Zawadi walibadilika, wakaachana na dawa za kulevya, pombe na marafiki wabaya. Walijiunga tena na kundi la vijana katika parokia ambapo walipata mashauri ya masuala ya kiroho na kijamii. Zawadi alisaidiwa na kanisa pamoja na familia yake mpaka akajifungua mtoto mrembo wa kike, Hope. Washauri, mapadre na wazazi wa Tarajio na Subira waliihakikishia familia hiyo kuwa wangeendelea kuisaidia kurejelea maisha yao adilifu ya awali. Familia yote ilimsaidia Zawadi kumlea Hope na furaha ikarejea tena katika boma la Tarajio na Subira.

## Amua: Utathmini wa hali halisi

Familia ni nguzo muhimu kwa kila mtu. Ni chanzo cha kila mmoja wetu cha uhai, upendo na malezi. Mtoto akizaliwa, jamii hupokea zawadi ya mgeni miongoni mwao na kuanza mara moja kumshirikisha kwa jamii. Familia ndiyo jamii asili ya kila mtu inayotuwezesha kutoa mchango maalumu na usiofidika kwa manufaa ya jamii. Familia inatambuliwa pia na Katiba ya nchi. Kifungu 45 kinaeleza kuwa familia ndicho kitengo cha asilia na kimsingi cha jamii na msingi muhimu katika mpangilio wa jamii, na itafurahia kutambuliwa na kulindwa na Serikali.

Iwapo Kanisa na Serikali zinatambua umuhimu wa nafasi ya familia, ni kanuni ya asili kwa familia kutekeleza kazi na majukumu yake ya kimsingi katika malezi ya watoto ili kukuza vipawa vyao, kuwawezesha

kutambua hadhi yao na kuwaandaa kukabili hali yao ya kipekee na ya kibinafsi maishani. Familia hujipata katika mazingira maalumu kutokana na mabadiliko ya kasi ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na imani za kidini. Isitoshe, majanga ya maradhi yameacha familia nyingi zimechanganyikiwa, zikisumbuka akili na kuvunjiwa matumaini. Nchini mwetu leo, familia zinakumbwa na shida zisizo na kifani, na jukumu la wazazi limevurugika kutokana na ushindani wa athari nyingine nyingi za ulimwengu. Mtazamo wa masuala ya dunia na mfumo wa maadili zinabadilika haraka kiasi kwamba wajibu wa wazazi umezidi kufifia.

Familia za siku hizi zinakumbwa na matatizo kama vile talaka, utengano, dhiki, kuzorota kwa uchumi, changamoto za malezi, ukosefu wa ajira, magonjwa, ulemavu, utumiaji mbaya wa dawa na pombe, kutawaliwa akili na kamari, na mimba za matineja. Shida nyingine ni vijana kupewa mafunzo ya siasa kali, kuwachafua na kuwatesa watoto, kuwafanyiza watoto kazi na kuwauza kimagendo, wazazi kutokuwa na wasaa wa kutosha kuwalea watoto wao na kuwapa mwongozo wa maadili yanayofaa, fujo za kinyumbani na visa vya watu katika familia kujitoa uhai. Hata hivyo, pana matumaini ya familia zote kurudi kwenye chaanzo na shabaha ya familia. Kanisa halifai kamwe kuyumba katika juhudi zake za kuitetea na kuilinda familia. Nayo jamii kwa jumla inapaswa kufikiria upya na kuandaa mikakati ya jinsi ya kuimarisha na kujenga taifa lenye watu wacha Mungu kuanzia katika familia.

Maaskofu Wakatoliki Kenya kwenye hotuba yao kwa taifa mnamo Agosti 29, 2020, walikariri umuhimu wa malezi yanayozingatia uwajibikaji. Malezi ni jukumu muhimu kwa mzazi yeyote na ni kazi inayohitaji maarifa, juhudi, kujitolea na uvumilivu. Uwepo wa baba na mama kwa pamoja ni nguzo muhimu katika kulea watoto. Maaskofu wanahimiza wazazi kuwafunza watoto wao kuanzia wakiwa wachanga kanuni zifaazo za uadilifu, imani na masuala ya uzazi, na wapige vita mafunzo na mifumo inayopinga familia na iliyo kinyume na mafunzo ya Kristo.

## Tafakari ya kiroho

Mwanzo 9:8-15
1 Petero 3:18-22
Marko 1:12-15

Familia imelengwa na mashambulizi mengi ya kimawazo kusudi kuiangamiza. Jaribio la kuwapokonya wazazi haki za kuwalea watoto

wao ni tishio kubwa kwa kiini cha familia. Hali hiyo inazoroteshwa na juhudi zinazofanywa kuimarisha utumiaji wa dawa za kupanga uzazi na utunguaji wa mimba miongoni mwa matineja. Tukiwa Kanisa, hatuna budi kupinga njama zote hizi za kuiangamiza familia. Msukumo mkubwa wa njama hizo ni ahadi ya kujilimbikia mali, ulafi na tamaa ya mamlaka.

Masomo ya leo yanazungumzia kuhusu kuangamizwa kwa dunia iliyotawaliwa na uovu na kutoa nafasi ya kuujenga ulimwengu mpya. Mafuriko yaliitakasa dunia iliyotawaliwa na dhambi na kutoa nafasi ya kizazi kipya cha watu. Ubatizo ni ishara ya mtu kuzaliwa upya. Injili inatwambia kwamba kuyashinda mauti kulianzia wakati Yesu aliyashinda maovu na nguvu zote za uovu. Tunahimizwa kuzitfuta nguvu za Kristo ili kuyashinda maovu maishani mwetu, hasa nguvu za kuyashinda majaribio.

Mwaka ujao tutawachagua viongozi. Tunapaswa kuanza kuwatambua wanaume na wanawake wanaojali familia. Tukifanya hivyo, tutakuwa na nafasi nzuri ya kupata viongozi wema. Ujumbe huu unapaswa kuwafikia wote wanaonuia kugombea uchaguzi. Hii ndiyo njia pekee ya kulishinda ovu la wasiothamini familia na uhai.

### Tenda: Maswali ya kuwazia

1. Ni vitishio gani vya kisasa vinavyoniathiri, familia yangu na jamii kwa jumla?
2. Una habari zozote kuhusu kampeni za kupotosha na ambazo zinatishia maadili ya familia katika eneo lako? Iwapo zipo, jadilianeni.

### Kujichunguza

1. Nimechangia kwa njia yoyote ile katika kuangamiza au kuimarisha familia?
2. Nimechangia katika kuimarisha maadili ya familia?
3. Nimeunga mkono mashirika yasiyo ya serikali, taasisi nyingine au watu binafsi wanasambaza mawazo potofu ya kigeni?

### Matendo yaliyopendekezwa

1. Jumuia itambue washauri kuzishika mkono familia zinazokabiliwa na changamoto.
2. Tambua, tangaza na uimarishe mipango ya maisha ya familia katika parokia, maeneo ya kuabudia na jumuia.
3. Kuanzishwa kwa mradi unaoongozwa na kanisa wa kutoa mashauri na nasaha kwa vijana.

# *Wiki ya Pili*

**VIJANA WETU, TEGEMEO LETU LA SIKU ZIJAZO**



## VIJANA WETU, TEGEMEO LETU LA SIKU ZIJAZO

### Tazama: Simulizi

Kazikwetu, kijiji kilichokuwa na miti na mimea mingi katika lokesheni ya Maji Matamu kilibarikiwa pia kuwa na mashamba yenye rutuba na vito vya thamani. Wakazi walitegemea uuzaji wa bidhaa tofauti kujipatia mapato yaliyowawezesha kuishi maisha mazuri na kupeleka watoto wao shuleni za kifahali.

Kijiji kilikuwa na jingine la kujivunia, kiwango thabiti cha maadili ambayo kila mmoja alibeba jukumu la binfsai kuyalinda. Wazazi na wazee wa kijiji walifunza vijana maadili hayo na kuhakikisha yanazingatiwa ipasavyo na kila mwanakijiji.

Umaridadi na utajiri wa Kazikwetu zilivutia wageni wengi waliotamani kufanya biashara au kujitafutia makao. Wageni walikifungulia kijiji kwa ulimwengu na kuwapatia vijana wake nafasi mpya. Upeo wao wa mawazo ulipanuka na kuwawezesha kuwa na mtazamo wa kilimwengu na kuwasiliana na wenzao nje ya kijiji. Maadili, kijana mzaliwa wa Kazikwetu, alikutana na kubadilishana mawazo na Raha, kijana ambaye wazazi wake walihamia Kazikwetu. Urafiki kati ya Maadili na Raha uliimarika na ikawa ni kawaida kuwa pamoja mara nyingi wakitazama filamu chafu na kusikiliza muziki wenye maneno yasiyofaa. Wakafanya mazoea ya kuhudhuria karamu ambazo hazikuwa na usimamizi wa kufaa na ambapo walitumia vibaya dawa za kulevya na pombe. Wakati mwingine ungewapata wakitazama boli pamoja na kutumia pesa zao za akiba kucheza kamari. Vijana wengine waliungana nao kushirika katika maovu na idadi ya marafiki zao ikaongezeka. Hatimaye, badala ya kutumia wasaa wao mwingi kusoma wakati shule zimefungwa, ikawa ni kuhudhuria karamu baada ya nyingine. Wakakoma kuhudhuria ibada za misa, wakapuuza majukumu yao nyumbani na wakahepa shughuli za jamii ya Kazikwetu. Karibu kila mtu aliyejali katika jamii hiyo akaanza kusikitikia hali ya vijana hao na kutaka hatua zichukuliwe kuwapiga msasa.

Wazazi wa Kazikwetu walikutana na wale wa Raha kujadiliana kuhusu mienendo mibaya ya Raha na athari zake kwa vijana wengine kijiji ambazo matokeo yake yalikuwa ni kuzorota kwa maadili na uzembe. Wazazi wa Raha walihisi hatari na wakaamua kuwasiliana na watawala wa kijiji ili kupatanishwa na jamii. Watawala waliitisha mkutano wa viongozi wa kidini, wazee na viongozi wa jamii, wazazi na vijana. Wazazi wa Raha walijaribu kumtetea mwanao wakidai tabia zake

na za wenzake zilikuwa shwari. Badala ya kutafuta jinsi ya kubadilisha mienendo yake, wakapendekeza kudhamini miradi kadhaa ya jamii kama vile elimu na shughuli nyingine za ustawi wa vijana. Viongozi wa kidini hawakuridhishwa na pendekezo hilo kwani hawakuwa na uhakika lingetoa suluhu kwa tatizo lililokuwepo. Walitaka kufafanuliwa ni shughuli zipi hizo ambazo vijana wangehusishwa, elimu ambayo wangepata na shabaha yake. Walitaka miradi ambayo ingeshirikisha jamii yote.

Kauli ya viongozi wa kidini iliwahamasisha wakazi wa Kazikwetu kusisitiza kupata ufafanuzi wa pendekezo la wazazi wa Raha. Walieleza wazi masikitiko na wasiwasi wao kuhusu tabia za Raha na kutaka ufafanuzi wa jinsi shughuli zilizopendekezwa zingesaidia kutatua tatizo za kuzorota kwa maadili miongoni mwa vijana. Wazazi wa Raha walielewa hisia za jamii, wakatambua hofu yao na wakaazimia kuunga mkono miradi ya mashauri na kubadili tabia za vijana. Hatimaye, Maadili alianza tena kushiriki kikamilifu katika miradi ya kanisa na akamshawishi Raha na marafiki zao wengine kushiriki. Talanta na ujuzi wa mambo tofauti ziliwawezesha kutumia vyema wasaa wa mapumziko, wakashiriki shughuli za kujenga jamii na wakajitwika majukumu ya familia zao.

## Amua: Utathmini wa hali halisi

Kufungwa kwa shule kwa muda mrefu kufuatia kuzuka kwa janga la COVID-19 kumefichua udhaifu wa malezi na taratibu za jamii, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa mkabala wa jumla wa ustawi wa watoto na vijana wakiwa nyumbani saa zote. Watoto wengi wamepoteza mwelekeo. Vijana wengi wamesukumwa kwa shamrashamra za ulevi na utumiaji wa dawa za kulevya, uhalifu, ukahaba na unajisi wa watoto. Idadi ya matineja waliotunga mimba imeongezeka kwa kasi ya kusikitisha.

Mapendekezo kadhaa ya kukabiliana na tatizo la mimba za matineja yametolewa, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa sera ya elimu pana ya uzazi. Sera hiyo ina mapendekezo yasiyokubalika na maelezo yasiyo wazi. Huenda wengine wakauliza elimu, hasa ya suala muhimu kama uzazi, sio jambo nzuri? Tukizingatia kauli hiyo, si basi elimu hiyo inafaa kuwa pana? Majibu yanategemea nia na anayelengwa.

Watetezi wa sera ya elimu pana ya uzazi wanasisitiza kuwa hiyo ndiyo njia bora zaidi ya kuzuia mimba za matineja na mbinu hatari za utoaji mimba. Wanahimiza mataifa kukubali sera hiyo ili:

1. Kuhakikishia watu wote dawa nafuu na thabiti za kupanga uzazi na elimu pana ya uzazi, bila kujali umri wao.

2. Kuhakikishia wote huduma salama za kutoa mimba na utunzaji wa kiwango cha juu baada ya kutoa mimba.
3. Kuheshimu haki ya wanawake kuwa huru kuamua kuhusu afya yao ya uzazi, na hivyo kutowashirikisha wanaume wenzao katika maamuzi hayo.

Maelezo ya umri ufaao katika sera hiyo si bayana. Wanaharakati wa masuala ya elimu ya uzazi wanatumia suala hilo kimkakati kutoa hakikisho wajualo si la kweli kuhusu usalama wa watoto wasio na hatia, ilhali ni wao wanaoamua maana ya umri ufaao. Watetezi wa haki za uzazi wanatumia suala la umri kuwahadaa walioazimia kulinda watoto na haki zao.

Suala la watoto kuzaa ni tatizo la kijamii linalopaswa kushughulikiwa na kila mtu binafsi mwenye akili timamu. Kila mshika dau katika jamii hana budi kuchukua hatua na kukomesha tatizo hilo. Kanisa, katika hati zake za mafunzo ya kijamii na nyaraka mbali mbali za maaskofu zimethibitisha utukufu wa maisha ya binadamu kutoka wakati mwanamke anatunga mimba mpaka mtu anapokufa. Hati hizo zinapinga hali halisi na ya kusikitisha ya kuua watoto kabla hawajazaliwa kama sulushisho la tatizo hilo. Tunapaswa kutilia mkazo jinsi ya kuzuia mimba za mapema kwa hatua dhahiri kama vile mashauri na mipango ya kubadili tabia, ustadi maishani na elimu ya uzazi.

Mambo mengine yanayohitaji kutiliwa mkazo ni masuala ya kijamii yanayosababisha umaskini, magonjwa, uzinzi, msukumo wa rika na wasiwasi miongoni mwa watu. Tunaweza kutambua njia za kuwaelimisha kuhusu mambo ya kimsingi wafaayo kuchagua maishani yao binafsi na ya familia. Tuunge mkono taratibu zinazowapatia makao na kuwakinga wanawake na watoto walio hatarini.

Kufuatia kufunguliwa tena kwa taasisi za elimu, vijana wanahitaji kujenga upya ndoto na mipango yao ya siku zijazo.

## Tafakari ya kiroho

Mwanzo 22:1-2.9a.10-13.15-18
Waroma 8:31b-34
Marko 9:2-10

Imani ni muhimu kwa uhai. Dhana hii ni kweli hata katika sayansi. Kila mmoja anahitaji kiwango fulani cha imani ili kupiga hatua katika utafiti wa kisayansi. Abrahamu alihitaji imani ili kuifuata barabara aliyoonyeshwa na Mungu; Wakristo pia wanahitaji imani ili kumfuata Kristo. Tunabadilishwa maishani kwanza kwa kuipitia njia ya msalaba na kwa kujiweka mikononi mwa Mungu. Msingi wa imani yetu ni mapenzi

ya dhati aliyonayo Mungu kwetu na yasiyo na masharti.

Kwa njia tofauti, masomo yote ya leo yanaangazia msalaba. Tunayatangaza maisha ya Yesu duniani kwa ulimwengu kama thibitisho la upendo wa Mungu kwetu baada ya kuutazama msalaba wa Yesu. Tunapaswa kuwafunza vijana wetu kuifuata njia ya msalaba. Ili kuyajenga maisha yao ya baadaye, wanapaswa kufahamu kwamba matendo yetu mengi huzaa tabia na mazoea ambayo hatimaye huumba hulka zetu na kuyaunda maisha yetu ya baadaye. Kuishi wakizingatia imani ni muhimu katika ujana wao. Vijana wanahimizwa kuwatii wazazi. Wanapaswa kukumbuka kwamba watakuwa na muda wao wa kuchukua maamuzi. Huu ni msalaba ambao hawana budi kujifunza kuubeba na kamwe hawatajuta maishani yao ya baadaye.

## Tenda: Maswali ya kuwazia

1. Janga la COVID-19 limefichua mapengo katika shughuli za vijana?
2. Unayo mapendekezo gani ya kusaidia kuziba mapengo hayo?
3. Tunawezaje kuirejesha nafasi ya familia na kuiimarisha ili ziwe mahali pa kufunzia watoto na vijana, kuhimiza na kuendeleza yote yanayothaminiwa na jamii?
4. Kanisa linaweza kuchangiaje katika juhudi za kuwajenga vijana katika jamii yetu?

## Kujichunguza

1. Nikiwa kijana, nimechagua kwa busara ninayoyaiga kutoka kwa wengine?
2. Nikiwa mzazi, nina uhusiano huru na watoto wangu vijana? Je, wananiamini kiasi cha kunifungulia roho zao?
3. Katika juhudi zangu za kumtafutia mtoto wangu nafasi, huwa ninajitwika mzigo wa kutafuta kwa kina historia za wanaowasaidia?
4. Je, tunawafahamu na kuwatumbua vijana katika jumuia yetu?

## Matendo yaliyopendekezwa

1. Kuwajenga na kuwainua vijana katika jumuia.
2. Kuanzisha miradi ya kuwashauri vijana katika parokia.
3. Kuchunguza kwa kina mapendekezo ya elimu pana ya uzazi, sheria zinazopendekezwa huku tukitilia maanani utata unaoingizwa makusudi.
4. Kuandaa shughuli za kuwawezesha vijana kutekeleza waliyojifunza katika Injili.

# *Wiki ya Tatu*

UFISADI NA UFUFUAJI WA UCHUMI



## UFISADI NA UFUFUAJI WA UCHUMI

### Tazama: Simulizi

Kijiji cha Ukweli na Haki kilitambulika kwa maendeleo yake na amani. Jamii yake ilisifika kwa bidii kazini na wengi wao walikuwa wafanya biashara za aina nyingi. Walishiriki katika maendeleo kwa kutumia mikopo na misaada kutoka kwa hazina wa Mazao kuimarisha miradi ya kuiinua jamii kiuchumi. Washika dau wote walijadili mapendekezo ya bajeti za miradi ya maendeleo na kutoa nafasi ya kupanga kwa utaratibu utekelezwaji wa mipango kwa manufaa ya wote.

Miaka kadhaa baadaye, uchaguzi wa uongozi wa hazina ya Mazao uliitishwa na kuvutia wagombeaji wengi. Haja ya baadhi ya waliojitokeza ilikuwa ni kupata nafasi ya kujinyakulia sehemu ya pesa za hazina hiyo. Wadhifa wa mwenyekiti ulivutia wagombeaji wengi waliotumia mbinu za kila aina kufanya kampeni, ikiwa ni pamoja na kuwahonga na kuwatishia wanakijiji. Matokeo yake yakawa ni kuibuka kwa ufuasi na siasa za kiukoo ambazo hazikuwahi kushuhudiwa hapo awali. Kampeni zikifikia ukingoni, ni wagombeaji wawili pekee waliokuwa bado mbioni. Mmoja alikuwa mhisani msifika na mzee wa mojawapo ya koo kubwa kijijini ambaye asili ya utajiri wake ilizusha mashaka. Wa pili alikuwa mwanamke mfanya biashara ambaye alikuwa na uhusiano mwema na wanakijiji. Alinoa maarifa yake ya biashara na kukuza mali kupitia kwa mikopo ya hazina ya Mazao tangu akiwa kijana. Alikuwa mhusika mkuu katika shughuli za kanisa la kwake, na alijali uwazi na uwajibikaji katika shughuli zake zote. Sifa hizo zilijidhihirisha katika kikundi cha akina mama kijijini ambapo alikuwa mtunza hazina. Uchaguzi ulipofanyika, mzee mhisani alishinda kwani alikuwa ametumia pesa nyingi kuhonga wapigaji kura, hasa wa ukoo wake, na alitumia pia wadhifaa wake kama mzee wa ukoo kuyumbisha matokeo.

Miaka miwili baadaye, idara ya utabiri wa hali ya anga ilionya kuhusu uwezekano wa kijiji kukabiliwa na janga la ukame na njaa. Wanakijiji wakahimizwa kuweka akiba za chakula. Wazee wa kijiji walikutana na wakuu wa idara zote husika, ikiwa ni pamoja na mwenyekiti wa hazina ya Mazao, kuijadili ilani hiyo. Mkutano uliazimia nafaka zaidi zinunuliwe ili kuimarisha akiba ya chakula kijijini na kuhakikisha kingetosha kwa wote. Pesa kutoka hazina ya Mazao zilitengewa mradi huo.

Kama ilivyotabiriwa, mvua za masika hazikunyesha na kijiji kikakumbwa na ukame na njaa. Mito na maeneo ya kuhifadhia maji

ilikauka na wanyama wakaanza kufa. Miradi kama vile mpango wa kuwalisha wanafunzi shuleni iliathiriwa. Wanafunzi wengi walilazimika kuacha kusoma na badala yake wakawa wanatafuta maji katika vijiji jirani kwa matumizi ya nyumbani na kunywesha wanyama. Ukame ulivyoendelea, wanakijiji walianza kufariki. Uongozi wa kijiji ulitaka kuelezwa na wasimamizi wa hazina ya Mazao ni kwa nini hakukuwa na chakula cha misaada ilhali pesa za zilishatengwa. Uchunguzi wa hesabu ulibaini kuwa mwenyekiti alikuwa amefuja pesa za miradi pamoja na za kukabiliana na ukame na njaa.

Ili kubadilisha hali ya mambo na kuzuia vifo zaidi kutokana na njaa, wazee walimwalika mwanamke mfanya biashara aliyebwagwa uchaguzini wa hazina ya Mazao asaidiane na wanakijiji. Akitumia mitandao yake ya kibiashara na shughuli nyingine, alipata misaada ya chakula ambacho kamati iligawia familia zote zilizoathrika pamoja na taasisi kama vile shule, makao ya mayatima na wazee. Wazee wa kijiji waliitumia fursa hiyo kutafuta suluhisho la kudumu. Waliitisha baraza la dharura kwa mafunzo kuhusu uongozi na uadilifu, uwajibikaji na hatua za kujikinga na mabadiliko ya hali ya anga. Wanakijiji walitambua makossa waliyoyafanya ya kumchagua kiongozi mfisadi kusimamia hazina ya Mazao na wakaamua kufanya uchaguzi mwingine. Walimchagua mwanamke mfanya bishara ambaye mwanzoni walikuwa wamemkataa. Msimamizi huyo mpya mara aliposhika hatamu za uongozi, aliweka mikakati mipya ya kuimarisha hatua za kuufufua uchumi na kujitosheleza kwa chakula. Kupitia kwa uongozi wake shirikishi na kutokana na uzoefu aliokuwa nao katika biashara, alihimiza uwekezaji anuwai na kujenga uhusiano mwema kati ya kijiji cha Haki na Amani na majirani zake, mitandao ambayo ilisaidia kukuza hazina ya Mazao na kurejeshea kijiji hicho sifa yake ya zamani.

## Amua: Utathmini wa hali halisi

Ufisadi uliomea mizizi na kuenea kote ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazokabili Kenya. Ufisadi ni utumiaji mbaya wa mamlaka ili kujinufaisha kibinafsi.

Katiba katika utangulizi wake inatambua maratajio ya Wakenya wote kwa Serikali iliyo na misingi bora ya haki za binadamu, usawa, demokrasia, haki za kijamii na utawala wa kisheria na inayowapatia uhuru na haki ya kuamua aina ya uongozi wanaoutaka na wakiwa wameshiriki kikamilifu katika kuiunda Katiba. Malengo hayo yanatimizwa kwa kuzingatia kanuni za uongozi bora, uadilifu, uwazi na uwajibikaji.

Katiba iliweka kanuni kadhaa kwa lengo la kubadilisha utawala na uongozi na pia kuwachunga maafisa wa umma. Kanuni hizo ni pamoja na Sura ya 6 kuhusu uongozi na uadilifu na Kifungu 10 kuhusu Maadili ya Kitaifa na Kanuni za Utawala.

Ripoti ya uchunguzi wa ufisadi ya Transparency International Corruption Perceptions Index ya 2019 imeiweka Kenya katika nafasi ya 137 kati ya nchi 180 fisadi dunini, thibitisho la jinsi Kenya inavyojikokota katika kupiga vita ufisadi na rushwa.

Kwenye jamii yetu leo, ufisadi ni swala linalojadiliwa katika sekta zote. Mashirika mengi ya umma na binafsi yanakabiliwa na tatizo la utoaji wa huduma duni au hata kushindwa kabisa kuhudumu. Mashirika ya umma na binafsi yanayopaswa kutekeleza kanuni za uadilifu na uwajibikaji yamehusishwa pia na ufisadi. Kiasi kikubwa cha pesa za umma na za mikopo kimepotelea katika mitandao ya ufisadi na rushwa, bila kujali kuwa tunazo sheria na sera za kupambana na ufisadi, kama vile Sheria ya Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi ya 2011, Sheria ya Uongozi na Uadilifu ya 2012, Sheria ya Kupambana na Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi ya 2003 na Sheria ya Maadili ya Maafisa wa Umma ya 2003. Ufisadi umekwamisha utoaji wa huduma muhimu katika serikali ya kitaifa na za kaunti. Madhara ya ovu hilo yamekuwa ni kuongezeka kwa pesa ambazo Serikali imekopa nchini na kutoka nje, utumiaji mbaya wa pesa za umma na utengaji rasilmali kwa miradi isiyo na manufaa kwa umma. Wakenya wengi wanaumia na mzigo huo utabebwa na vizazi vijavyo.

Tume ya Kupambana na Ufisadi (EACC), Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP), Idara ya Uchunguzi wa Jinai (DCI) na Mahakama, zimepiga hatua za kutia moyo katika vita dhidi ya ufisadi. Tumeshuhudia siku za karibuni maafisa wengi wakuu wa umma wakishtakiwa na wengine wakipokonywa mali za umma walizojinyakulia au mali walizojipatia kwa mapato ya kihalifu. Kadhalika, uchunguzi wa maisha ya watumishi wa umma uliofanyika 2019 ulithibitisha kuwa baadhi yao hawangeeleza jinsi walivyojipatia mali walizonazo. Mfumo wa sasa wa kuwakinga wanaofichua ufisadi chini ya sheria ya kupambana na ufisadi na zile za kuwalinda mashahidi unapaswa kutekelezwa kikamilifu. Kadhalika, Wakenya wafahamishwe kuhusu mfumo huo, kwani wengi huogopa kufichua ufisadi kwa kuhofia kuumizwa.

Vita vya ufisadi ni jukumu la pamoja na halifai kuachiwa mashirika ya serikali pekee. Wananchi wana jukumu la kutekeleza, hasa kutambua wafisadi, kuchunguza, kukagua na kupiga ripoti matendo ya kifisadi

na kuwafichua wahusika. Kanisa Katoliki linahusika katika shughuli mbali mbali za kupigana na ufisadi likizingatia mafunzo yake ya kijamii yanayokariri kwamba ufisadi ni dosari kubwa katika mfumo wa kidemokrasia na ni ovu linalopaswa kuwasikitisha wote katika jamii. Ufisadi husaliti kanuni za maadili na ada za haki kwa jamii. Huwafanya raia kutoridhishwa na kutoamini mashirika ya umma. Huharibu kabisa jukumu la mashirika wakilishi, na hasa iwapo wenye uwezo wa kuamua mkondo wake wa utendakazi ni walafi na tamaa zao zinazuia kupatikana kwa manufaa kwa wengi. Baba Mtakatifu Francis alipozuru Kenya mnamo 2015, aliwahimiza wote kuepuka ufisadi kwani hiyo ni njia ya mauti.

Mnamo Oktoba 5, 2020, Kanisa lilianzisha kampeni ya kitaifa kupigana na ufisadi yenye maudhui *Ninapinga ufisadi … Tuivunje Minyororo ya Ufisadi …* Ikiongozwa na maaskofu Wakatoliki Kenya, kampeni inahimiza watu binafsi kupiga ufisadi vita kwa kuamsha dhamiri za waumini na watu wenye mapenzi mema kuimarisha moyo mpya unaoongozwa na uaminifu na uadilifu.

## Tafakari ya kiroho

Kutoka 20: 1-17
I Wakorintho 1:22-25
Yohane 2:13-25

Maudhui ya leo ni kuhusu kuijenga hekalu mpya mahala pa ile ya zamani. Kufuatia kufunguliwa kwa makanisa baada ya kuondolewa kwa marufuku ya kukabiliana na maenezi ya COVID-19, tunageuzwa kuwa viumbe vipya. Kwaresima ni msimu wa kujitakasa. Paulo anatuhimiza tusiwe na hekima kama ya Wayahudi na Wagiriki. Kafara tunayotoa ni lazima itakase dini yetu na kutuondolea madhehebu yasiyo na uhusiano wowote na kumpenda Mungu na majirani zetu. Janga la COVID-19 lilifichua dosari nyingi katika maisha yetu ya Kikristo na kuweka wazi vile hatujajitayarisha. Wanafunzi, walimu katika shule za binafsi na biashara ndogo hasa karibu na shule ziliathirika zaidi. Wazazi na washika dau waliteseka kimawazo, kifedha na vinginevyo kutokana na vyuo kufungwa kwa muda mrefu.

Mtakatifu Paulo anatuonya kwamba kupenda sana pesa ni chanzo cha uovu wote (1 Timotheo 6:10). Kiini cha ufisadi ni ovu la ulafi ambalo limepenya nyanja zote za jamii, ikiwa ni pamoja na waumini. Vita dhidi ya ufisadi, sawa na kauli mbiu aliyotoa nabii Amos kwa watu wake kwamba

tusichoke kupigana na aina zozote za manyanyaso, na hasa kuzuia fukara na wanyonge wasipate haki. Sawa na tunavyojifunza katika hotuba mlimani, huenda pakawa na gharama ya kurejeshea wanyonge na maskini haki lakini tukifanya hivyo, zawadi inatusubiri: "Heri wanaoteswa kwa sababu ya kufanya atakavyo Mungu, maana ufalme wa mbinguni ni wao." (Mathayo 5:10).

## Tenda: Maswali ya kuwazia

1. Miaka 10 baada ya Katiba mpya kuzinduliwa, tumepiga hatua gani za kuridhisha kwenye vita ya ufisadi? Ni mapengo gani yaliyopo bado?
2. Kampeni ya Kanisa Katoliki kupigana na ufisadi imepata mafanikio gani nchini? Ni mapengo gani yanahitaji kuzibwa?
3. Tunaweza kufanya nini kama jumuia ndogo au parokia kuziba mapengo hayo?
4. Ni hatua gani nyingine ambazo mashirika ya kidini yanapaswa kuchukua katika kupigana na ufisadi?

## Kujichunguza

1. Nimejitolea binafsi kupigana na ufisadi?
2. Katika shughuli zangu za kila siku, ninahimizaje ama kushiriki vipi katika aina yoyote ya ufisadi?
3. Nikiwa mzazi/mlezi, ninawapasha vipi watoto wangu maadili ya kupigana na ufisadi?

## Matendo yaliyopendekezwa

1. Kujitolea kibinafsi kupigana na ufisadi kuzingatia Sura ya 6 ya Katiba na kampeni ya maaskofu Wakatoliki dhidi ya ufisadi.
2. Kuhimiza na kuunga mkono kuchaguliwa viongozi kuzingatia uadilifu katika ngazi zote za uongozi.
3. Matembezi ya amani mnamo Siku ya Kimataifa ya Kupigana na Ufisadi (Desemba 9).

# Wiki ya Nne

USALAMA



## USALAMA

### Tazama: Simulizi

Milki ya kifalme ya Kwetu Salama katika Jamhuri ya Amani ni eneo lililofurahia amani na maendeleo. Miradi ya kubadilisha maisha ya raia wake kijamii na kiuchumi ilitilia mkazo uzalishaji mali, uvumbuzi na ubunifu. Ghafla, maendeleo katika nchi hiyo yakatishiwa na kuzuka kwa ugonjwa ajabu wa virusi vya kuambukizana.

Majuma kadhaa baada ya kuripotiwa kesi ya kwanza ya ugonjwa huo wa virusi ulioitwa *Karibiaufe*, Kwetu Salama ikatangazwa kuwa eneo la hatari. Ili kukabiliana na maenezi ya *Karibiaufe*, uongozi wa Amani uliweka vikwazo, ikiwa ni pamoja na marufuku ya kuingia au kutoka Kwetu Salama na sehemu nyingine hatari, kufungwa kwa shule na vyuo na kutangazwa sheria za kutotoka nje usiku. Raia wote waliagizwa kufanyia kazi nyumbani, isipokuwa waliokuwa wakitoa huduma muhimu.

Marufuku na sheria hizo nusura zikwamishe uchumi wa Kwetu Salama na kuwaacha wenyeji wengi bila njia ya kujipatia riziki wala matumaini maishani. Hatua za kuilinda jamii na kuwakinga wakazi hazikuwaletea manufaa mengi kwani zilikumbwa na tatizo la ufisadi na rushwa. Wakazi walichoshwa na vikwazo walivyowekewa na wakaanza kuvipuuza, huku wengine wakivunja maduka na majumba mengine ya biashara na makao wakijitafutia riziki. Visa vya fujo za kikabila vilizuka kutokana na mizozo ya zamani ya mashamba, uvamizi wa misitu na wizi wa mifugo. Kambi za kisiasa ziliibuka kwa vile uchaguzi wa kitaifa ulikuwa karibu kufanyika. Visa vya uhalifu pia viliongezeka kwani wengi walikuwa wamepoteza riziki zao. Makundi ya kigaidi kutoka Shidatupu, nchi jirani iliyokumbwa na misukosuko, yalipata mahala pa kuendeshea matendo yao ya kikatili miongoni mwa wakazi wa Kwetu Salama. Kadhalika, walipata fursa nzuri ya kutoa mafunzo ya itikadi kali na kuandikisha vijana wengi kwa mitandao yao. Usalama katika Kwetu Salama ulizorota, hali iliyoendelea hata baada ya janga la *Karibiaufe* kuthibitiwa.

Viongozi wa kidini na wawakilishi wa jamii za wakazi waliungana na kubuni baraza lililoleta pamoja viongozi mbali mbali wa kidini ili kupigana na misukosuko na uvunjaji wa haki. Makundi hayo mawili, Amani Interfaith Forum na Kwetu Salama Interfaith Council of Clerics, yalifanya kazi kwa pamoja kurejesha na kupigania kuimarishwa kwa usalama.

Makundi ya usalama na amani mashinani yalibuniwa na kuleta pamoja uongozi wa milki hiyo, viongozi wa kidini na wawakilishi wa makundi ya kijamii. Makundi mengine ya jamii yaliundwa ili kupigana na ufisadi katika miradi ya kulinda jamii, kuimarisha hali yao ya kiuchumi na kuwezesha kila mmoja kujitegemea. Milki hiyo ilitumia huduma ya Linda Jamii kumaliza mitandao ya fujo na migogoro, na kurejesha amani na usalama katika Amani.

Kwetu Salama na jamhuri yote ya Salama zilirejelea hali yake ya amani na maendeleo na raia wake wakatangazwa kuwa watu wenye furaha zaidi na waliojawa na matumaini kote katika kanda.

## Amua: Utathmini wa hali halisi

Kwenye utangulizi wa Katiba ya nchi, inatambuliwa kwamba Wakenya wanajivunia tofauti zao za kikabila, kitamaduni na kidini na kuazimia kuishi kwa amani na umoja wakiwa taifa moja huru. Sheria kuu inatambua pia kujitolea kwa Wakenya kukuza na kuhifadhi maslahi ya watu binafsi, familia, jamii na taifa.

Hata hivyo, mnamo miaka ya karibuni, Kenya imekumbwa na tatizo la siasa za kibinafsi na ufisadi ulioenea katika serikali ya kitaifa na za kaunti. Matokeo yamekuwa ni kupunguka kwa nafasi za raia kujiendeleza, kuzorota kwa usalama, kuongezeka kwa uhalifu na makundi ya kigaidi.

Kuzorota kwa hali ya uchumi kutokana na janga la COVID-19 kumepotezea wengi riziki, kumesababisha ongezeko la watu wasio na ajira, kupandisha viwango vya umaskini na kuzorotesha usalama wa jamii. Vijana Wakenya waliokata tamaa maishani, ikiwa ni pamoja na wanafunzi waliochoka kukaa nyumbani kwa muda mrefu, wamejiunga na makundi ya kihalifu wakijaribu kujitafutia riziki angalau wagharamie mahitaji yao muhimu na ya wanaowategemea.

Hatua za Serikali za kulinda jamii zinakumbwa na ufisadi na hazijafaidi makundi yanayolengwa. Mipango ya usalama katika jamii, kama vile juhudi ya Nyumba Kumi, inayumba. Dawa za kulevya zinapatikana kwa urahisi kwa watumiaji wazoefu ambao idadi yao inaongezeka kila uchao na kusababisha kuongezeka kasi kwa visa vya uhalifu na haja ya kupata pesa za kudumisha uzoefu huo wa mihadharati.

Mitandao ya kigaidi inatumia udhaifu na hali ya kukata tamaa ya vijana Wakenya kusambaza itikadi kali na kuwasajili kujiunga na mashirika yao kwa ahadi ya kupata mali na ufanisi kwa wanaosajiliwa na familia zao pia.

Hatua zifuatazo zinapendekezwa ili kukabiliana na changamoto za usalama zinazokumba nchi:

1. Kufanyia mabadiliko shughuli za kulinda usalama wa nchi ili kuhakikisha zinazingatia hadhi, usawa na haki za binadamu kulingana na Kifungu 28 cha Katiba.
2. Kupiga vita ufisadi katika mashirika ya umma na ya binafsi ambayo yamechangia katika kutofanikiwa kwa juhudi za Serikali za kulinda jamii na kuiinua kiuchumi, na kwa kuwezesha magaidi kupenya na kupanua mitandao yao katika Kenya.
3. Kuimarisha ugatuzi na ushirika wa raia, hasa katika taratibu na shughuli za kuinua kiwango cha usalama na kukabiliana na uhalifu katika ngazi za jamii.
